NIKOFITI Na MAARIFA PESA

Muongozo wa kifedha kwa kila mtafutaji

TBA
TANZANIA BANKERS ASSOCIATION

HAKIMILIKI

NIKOFITI NA MAARIFA PESA
Kitabu cha Elimu ya Fedha kwa wajasiliamali wadogo Tanzania
© 2026 Chama cha Mabenki Tanzania (TBA). Haki zote zimehifadhiwa.
ISBN: 978-99975-78-27-3
Kimechapishwa nchini Tanzania
Tovuti: www.tanzaniabankers.org

Chapisho hili limetengenezwa kama nyenzo ya kielimu iliyoagizwa na Chama cha Mabenki Tanzania.

Hakuna sehemu yoyote ya chapisho hili inayoweza kutajwa, kuhifadhiwa kwenye mfumo wa kurudisha kumbukumbu, kusambazwa au kutolewa kwa mtindo wowote au kwa njia yoyote; ya kielektroniki, ya mtambo wa kunakili, kurekodi au vinginevyo bila ruhusa ya maandishi ya awali kutoka kwa Chama cha Mabenki Tanzania, isipokuwa kwa dondoo fupi zinazotumika katika uhakiki, utafiti wa kielimu au matumizi mengine yanayoruhusiwa chini ya sheria husika za hakimiliki. Wahusika wote katika hadithi na vielelezo wanalindwa na hakimiliki. Utoaji wowote usioidhinishwa au matumizi ya kibiashara ni marufuku.

SHUKRANI

Chama cha Mabenki Tanzania (TBA) kwa kuagiza kutengenezwa kwa chapisho hili na kwa nia yake thabiti ya kuboresha uelewa wa masuala ya fedha miongoni mwa Watanzania.

Mwandishi wa kitabu hiki: Yasinta Wandiba

Mchoraji: Ally Lupatu

NIKOFITI NA MAARIFA PESA

Jarida la elimu ya fedha kwa ajili ya watanzania wote.

Jarida hili limeandaliwa kwa hisani ya Tanzania Bankers Association (TBA) – Kwa ajili ya wafanyabiashara/wajasiliamali wadogo ;mamalishe, madereva bodaboda, mafundi mbalimbali na wachakalikaji wote ili waweze kusimamia fedha zao kwa kujiamini.

MAMBO YA KUZINGATIA

WEKEZA NA KUKUA

Rahisisha mahitaji yako. Tumia kiasi kidogo zaidi ya kile unachoingiza, kisha ruhusu muda ufanya mabadiliko yake.

PESA NA FIKRA

Mafanikio ya kifedha hayahusu unachoki-jua bali yanahusu zaidi mwenendo wako binafsi.

TUMIA KWA FURAHA

Kata matumizi yasiyo ya lazima, ili uweze kutumia zaidi kwa uhuru katika yale yanayo kupasa yaliyo muhimu na yalazima.

NAMNA YA KUSOMA JARIDA HILI

HALI HALISI: Tukio la kifedha kutoka kwenye maisha halisi.

CHANGAMOTO: Mahali mambo yanapoenda mrama.

HATUA: Jambo la busara la kufanya.

MATOKEO: Maisha yanakuwa bora.

Huhitaji kuwa tajiri ili uanze. Unahitaji tu kuanza anza hapo hapo ulipo.

Kutana na Mtaa wa Faraja

Majirani sita, harakati sita na mzee mmoja mwenye hekima. Shida zao nyingi zinaweza kufanana na zako...

PAPA MFUMO

Mmiliki wa duka mwenye hekima, aliyejaa methali na ushauri wa busara.

DITO

Anauza vocha na kava za simu, Kijana mdogo mwenye njaa ya mafanikio anayeota utajiri wa haraka.

SKUDU

Dereva wa bodaboda na bajaji, kasi yake barabarani ndio hivyohivyo ilivyo kasi yake ya kutumia pesa.

ASHA

Fundi cherehani, anajiwekea akiba kimyakimya kwa ajili ya ada ya shule ya watoto wake.

BI KIJUMBE

Muuza mboga , anaendesha kikundi cha VICOBA cha mtaani na shangazi wa kila mtu.

TUMA

Mama lishe, anapika chakula kitamu sana lakini faida yake inaendelea kutoweka.

YALIYOMO

Kipato na bajeti....01
Huduma ya kibenki....06
Miamala ya simu....08
Hekima ya kukopa....10
Bima....13
Uwekezaji....16
Hela ya biashara....19
Utapeli na uhalifu....21
Siku zijazo....23
Msimu mmoja baadae....25
Kanuni 10 za pesa....26

KIPATO NA BAJETI

HALI HALISI:

CHANGAMOTO:

Jioni Tuma amefunga biashara na kuhesabu mapato yake.

TUMA ANAAMUA KWENDA KUMTEMBELEA PAPA MFUMO KUPATA USHAURI.
"Haiwezekani Papa Mfumo, kuna mkono wa mtu. Elfu tatu Kweli!! Mauzo ya siku nzima nimepata elfuu tatu! Si sawa,"
"Pesa bila mpango, ni sawa na kubeba maji kwa mikono. Mpaka unafika nyumbani, yametoweka yote."
HATUA:
"Ipe kila shilingi kazi ya kufanya kabla haijatoka mkononi mwako mwanangu. Kila shilingi ipate kazi ya kufanya kama ifuatavyo."
!

MAHITAJI YA LAZIMA. MAHITAJI YASIO LAZIMA. AKIBA.

MAHITAJI YA LAZIMA 50% - Kodi, chakula, mavazi, nauli, ada za shule malipo ya lazima kabisa.
MAHITAJI YASIO YALAZIMA 30% - Soda, mitoko ya usiku, nguo mpya – mambo mazuri kuwa nayo lakini si ya lazima.
AKIBA 20% - Jilipe mwenyewe kwanza, kabla ya kitu kingine chochote.

HALI HALISI
"Eti Benki? Ah wapi Pesa zangu ziko salama hapa hapa chini ya godoro langu. Babu aliweka hapo, baba akaweka hapo, mimi ni nani kupingana na enzi"
CHANGAMOTO
"Duh! nilijiwekea hapahapa kiakiba changu...lakini sasa mara binamu akaniazima, nyingine nikanunua vitu yani yani pesa haikai kabisa jamani."
IMETOWEKA
Ni kweli, Pesa taslimu iliyopo nyumbani, haikai. Inavuja kimyakimya na wala haiongezeki kamwe.
HATUA:
"Kwenye akaunti, pesa yako iko salama na inawezakukuwa wakati umelala."

MBEGU MOJA HUZAA NYINGI

Muda + Riba = Mavuno kamili
Hii ni riba ya mseto – Kwa maana ni pesa inayozalisha pesa nyingine.
DHARURA Ugonjwa, matengenezo, miezi migumu — akiba ndio amana yako ya dharura.
MALENGO YAKO Pikipiki, ada za shule, genge kubwa zaidi — kuweka akiba hufanya ndoto kuwa kweli.
AMANI YA NAFSI Pesa iliyopo benki inakuwezesha kulala bila wasiwasi.

MATOKEO:

"Hata iwe 2,000/= kwa wiki! Akiba haiozi kamwe!"

JILIPE MWENYEWE KWANZA

Weka akiba muda uleule pesa inapoingia sio "kile kinachobaki" mwishoni mwa mwezi, kwa sababu hakuna kinachobaki.

IFANYE IWE YA KIOTOMATIKI

Weka mwendelezo wa kudumu wa kujiwekea pesa benki moja kwa moja au tumia njia za kidigitali kama kupitia mitandao ya simu ili kiasi kidogo kihamie kwenye akiba kila wiki bila wewe kufikiria.

wiki Hii: Fungua akaunti ya akiba au kwenye mtandao wowote wa simu na uweke **5,000/=** yako ya kwanza.

DONDOO ZA KIBENKI

FUNGUA AKAUNTI KWA HATUA 3

1. Leta NIDA / Vitambulisho vyako + namba ya simu.
2. Jaza fomu fupi kwenye tawi au kwa wakala.
3. Pata akaunti yako na kadi ya ATM papo hapo

PIN = SIRI (SECRET)

Usimwambie mtu yeyote **PIN** yako - awe rafiki au mtu anayedai kuwa “mfanyakazi wa benki”. Funika sehemu ya namba unapoingiza namba yako ya siri.

KAGUA MAJIBU YA UJUMBE (ALERTS)

Hifadhi risiti na usome kila ujumbe wa SMS unaoingia.Utagundua kama kuna kosa lolote kwa haraka. Elimu ya Msingi ya Benki

DONDOO ZA KIBENKI



AKAUNTI ZA BENKI NI RAHISI NA NAFUU

Benki nyingi zinatoa akaunti za gharama nafuu au zisizo na masharti magumu kwa akaunti ya kiwango cha chini cha pesa. Ulizia akaunti kwa ajili ya kuweka akiba au kwa wafanyabiashara wadogo wadogo.

DONDOO ZA KIBENKI

TUMIA PROGRAM YA SIMU AU USSD kama huna simu janja. Piga namba za ussd za benki husika. Kagua salio, tuma na uweke akiba bila kusafiri.

“Usalama wa mali ni hekima.” Kuweka pesa yako mahali salama ni hekima ya kweli. **WIKI HII:** chukua NIDA yako uende benki au kwa wakala na ufungue akaunti.

MIAMALA YA SIMU: LIPA TUMA! TUMA!

Pesa ya kwenye simu ni ya haraka na ina nguvu lakini kasi hiyo ina pande mbili. Kubonyeza mara moja bila umakini na pesa inakuwa imetoweka.

MIAMALA YA SIMU

Tuma kwa: NEEMA M. SAHIHI (✓)

"Kila mara kagua jina linalotokea kabla hujatuma pesa. Namba inaweza kukudanganya lakini jina haliwezi."

KABLA HUJABONYEZA KUTUMA

- **NAMBA:** Iandike mara mbili, isome tena kwa kurudia.
- **JINA:** Je, linafanana na muhusika?
- **KIASI:** Ziro zipo sahihi? Zihesabu.

JUA MAKATO NA VIWANGO VYA KUTUMA

Kutuma na kutoa kunagharimu ada ndogo.
Kagua kabla na sio baada ya kutuma pesa kwenye simu

PIN NA OTP = USIMWAMBIE MTU YEYOTE

Hakuna wakala au benki ya kweli itakayo kuomba PIN au namba yako ya siri ya muda (OTP). Mtu yeyote anayefanya hivyo ni mwizi, zuia hapo hapo.

IMETUNZWA KWA NJIA YA MITANDAO YA SIMU

"Jina limethibitishwa, bili imelipwa na hata ninaweka akiba moja kwa moja kUPITIA laini yangu ya simu sasa hivi!"

WEKA AKIBA KWENYE LAINI YAKO YA SIMU

huduma kama hizo zinakuruhusu kufungua akaunti ya akiba na hata kupata riba moja kwa moja kutoka kwenye simu yako.

SOMA KILA UJUMBE Kila muamala unatumiwa SMS. Zifunge na kuzitunza. Hizo ni risiti zako za bure na Ishara ya mapema ya kukutahadharisha dhidi ya utapeli.
"Hakiki kabla ya kuidhinisha."
Fuatilia kwa makini na ujiridhishe kabla hujachukua hatua.

Muamala: soma **JINA la uthibitisho** kwa sauti kabla hujabonyeza, ilikujiridhisha kabla ya kutuma.

KUKOPA KWA BUSARA (Majaribu ya Skudu)

MKOPO HARAKA! 50% kwa wiki

"Inabidi nipate simu kali ya kisasa na mimi. Na huyu jamaa anakopesha simu kwa kianzio cha shilingi 10,000 tu. Akah raha nijipe mwenyewe, kwani 10,000 kitu gani."

MTEGO! MTEGO!

(Majaribu ya Skudu)

NGAZi AU MNYORORO?

Mkopo unanunua pikpiki ya pili → unaingiza pesa kila siku unajilipa wenyewe = **ngazi**
Mkopo unanunua anasa → riba kubwa → hasara = **mnyororo**

DENi ZURi

Unanunua CHOMBO/ KITU kinachoingiza pesa kama bajaji, cherehani au mzigo wa biashara. Kinajilipia chenyewe.

DENi BAYA

Kukopa kwa ajili ya anasa/ na mambo yasio lazima kwa riba kubwa. Kitu hicho kinaisha au kuchakaa lakini deni linabaki palepale.

EPUKA MATAPELi NA KAUSHADAMU

Epuka Masharti yasiyoeleweka au viwango vya riba vya kutisha na vitisho.
Tunashauriwa kutumia benki, SACCOS au VICOBA.

KUKOPA KWA BUSARA (Muendelezo)
Pikipiki ya 2

MATOKEO

"Mkopo mdogo wa benki ulinunua bodaboda ya 2 inajilipia yenyewe kila siku.

SOMA KIWANGO HALISI CHA RIBA
Ulizia kiasi JUMLA utakachorudisha, na sio tu kile kiwango cha kila mwezi. Linganisha wakopeshaji na zingatia Kiwango cha riba kilicho wazi na kilichoandikwa ni ishara nzuri.

KOPA ILI KUJENGA
Kopa tu kwa ajili ya vitu vinavyoingiza pesa au vile unavyovihitaji kwa dhati, na kopa kiasi unachoweza kurudisha kwa urahisi tu. "Akopaye kwa busara, hulipa kwa raha."

KABLA YA MKOPO WOWOTE JIULIZE:
je, ni ngazi au mnyororo? Kama ni mnyororo usikope usikope.

BIMA

(Majanga yanapotokea)

MOTO! MOTO!

HALI HALISI

CHANGAMOTO

Huwezi kuzuia siku mbaya zisitokee, Lakini unaweza kuzizuia zisikuangamize. Ngao hiyo inaitwa bima.

HATUA



NGAO TATU ZA THAMANI ZA KUWA NAZO

AFYA: Mifuko ya bima ya afya ya jamii (CHF / iCHF) na NHIF inagharamia matibabu ili ugonjwa usimalize pesa zako.

MAISHA: Kiasi kidogo cha mchango kinawezesha familia yako kutunzwa endapo kitu kikikutokea.

MALI / BIASHARA: Kinga ya genge lako,duka, bodaboda au mazao, dhidi ya majanga ya moto au ajali.

MATOKEO

ANZA NA AFYA

Ndio dharura inayotokea mara kwa mara. Ulizia katika ofisi ya kata au hospitali kuhusu CHF / ICHF kwa ajili ya familia nzima. Vumbua kilichofichwa. Jua ni vitu gani mpango wa bima yako unavilipia na vipi hulipii.

Uliza maswali kabla hujasaini wakala mzuri atafurahia kuyajibu. "Kinga ni bora kuliko tiba."
MWEZI HUU: ulizia kuhusu bima ya afya ya jamii kwa ajili ya familia yako.

UWEKEZAJI (Mtego wa kutajirika haraka)

"Umesema ukiweka **100,000** napata **1,000,000**? Ah na mimi nautaka huo mchezo. Namimi **NIMO!** Niunge"

ONGEZA PESA ZAKO MARA DUFU KWA SIKU 7!

CHANGAMOTO

"Daima Pipi tamu ndio huozesha meno. Huo ni mtego huo sio uwekezaji."

Hilo ni kweli kabisa, kuweka akiba kunatunza pesa yako salama. Kuwekeza kunaisaidia kukua taratibu kwa miaka mingi na kwa uvumilivu. Mtu yeyote anayeahidi utajiri wa haraka anauza uongo."

KUWEKA AKIBA dhidi ya KUWEKEZA
WEKA AKIBA = sanduku salama la kuaminika, lipo siku zote
KUWEKEZA = kupanda mbegu

HATUA

WEKA AKIBA kwa ajili ya USALAMA
Dharura na malengo ya karibu. Unataka pesa hii iwe salama na tayari? Basi kukua taratibu kunatosha.

WEKEZA kwa ajili ya UKUAJI
Pesa ambayo utaiwekeza kwa miaka mingi. Kubali kupanda na kushuka; lenga mavuno makubwa zaidi.

NJIA ZA KUWEKEZA NCHINI TANZANIA

1. SACCOS / VICOBA
2. HATI FUNGANI ZA SERIKALI
3. HISA (DSE)
4. MIFUKO YA UWEKEZAJI WA PAMOJA ; UTT

Licha ya urahisi na usalama zaidi, utapanda daraja kuelekea uwekezaji wenye ukuuaji wa faida kubwa zaidi.

ANZA KIDOGO, ANZA SASA
Unaweza kuanza mfuko wa uwekezaji wa pamoja (UTT) au SACCOS kwa pesa kidogo sana.
Mawakala walioidhinishwa watakusaidia kununua hisa au hati fungani katika Soko la Hisa la Dar es salaam (DSE) huitaji kuwa tajiri kuanza.

TAWANYA UWEKEZAJI WAKO
Usiweke mayai yote kwenye kapu moja. Mchanganyiko ni mzuri wekeza kwenye; SACCOS, hati fungani ya serikali, mifuko ya uwekezaji wa pamoja hii hupunguza makali pale sehemu moja inaposhuka.

UWEKEZAJI
Hisa = kipande cha kampuni moja, Mifuko ya uwekezaji ya pamoja = kipande cha kikapu kizima cha uwekezaji mbalimbali na hili ni chaguo salama zaidi kwa wanaoanza. Mawakala katika Soko la Hisa la Dar es Salaam (DSE) sasa hivi wanaweza kukuhudumia kutoka mahali popote nchini.

MATOKEO

Mifuko ya uwekezaji ya pamoja INAKUA

KANUNI TANO ZA KUWEKEZA

1. ANZA KIDOGO, Anza na kile ulichonacho.
2. DUMU KWA MUDA MREFU, Miaka sio siku wala mwezi
3. TAWANYA, Usiweke kwenye kikapu kimoja kamwe.
4. PUUZA KELELE, Ushauri wa kupata pesa haraka ni mitego.
5. PUNGUZA GHARAMA. Makato makubwa yanakula faida.

"Subira huvuta heri."
ANZA uwekezaji mdogo wa kila mwezi: Hisa, SACCOS au mfuko wa uwekezaji wa pamoja badala ya kukimbizana na utajiri wa haraka.

PESA ZA BIASHARA (Mfuko mmoja wa Tuma)

Wakati pesa ya biashara na pesa ya nyumbani zinapochanganyika, faida inakuwa kama jini unaisikia wakati mwingine, lakini huwezi kuishika kamwe.

PESA ZA BIASHARA (Muendelezo)

BIASHARA | NYUMBANI

HATUA

KITABU CHA KUMBUKUMBU CHA KILA SIKU

PESA INAYOINGIA
PESA INAYOTOKA

VIBUNDA VIWILI VYA PESA

Tenga kabisa pesa ya biashara na pesa ya nyumbani, kwenye akaunti mbili tofauti.

JILIPE WEWE

Chukua "mshahara" uliojiwekea wa kila wiki, usitoe pesa ya akiba au kuchukua pesa Fulani kwa ajiliya kila haja ya nyumbani.

ANDIKA CHINI

Nukuu kila mauzo yanayoingia, kila gharama inayotoka na ufanye hivyo kila siku. Hivi ndivyofaida itaonekana wazi.

PESA ZA BIASHARA

MATOKEO

"Kaah kweli, Sasa hivi ninaona faida yangu halisi na ninawekeza tena ili kukuza biashara yangu!"

FAIDA DHAHIRI!

JUA NAMBA ZAKO

Faida = mapato yote ya mauzo yanayopatikana baada ya kutoa gharama za bidhaa na gharama zote za uwendeshaji, daftari la kumbukumbu huonesha kwa uwazi.

WEKEZA TENA ILI KUKUA ZAIDI
Rudisha sehemu ya faida kwenye mtaji zaidi au bidhaa bora zaidi. Hivyo ndivyo mtaji mdogo unavyokuwa biashara kubwa ya kweli.   "Biashara bila hesabu ni hasara."

KESHO: Chukua daftari na uandike kila shilingi ya biashara inayoingia na kutoka.

UTAPELI NA UHALIFU (Mtego ;Umeshinda)

UMESHINDA: 5,000,000= Tuma ada ya 50,000/= kwanza!

UTAPELI NA UHALIFU

JUA MITEGO YA KAWAIDA

1. "UMESHINDA!" Lipa ada ili kupata zawadi
2. "WAKALA FEKI" Mchezo wa kurudisha pesa / kutuma muamala kimakosa
3. "ONGEZA PESA MARA DUFU" Mipango ya Piramidi na Ponzi
4. "KUBADILISHA LAINI (SIM SWAP)" Wanaiiba namba yako
5. "VIUNGO/LINKI MBAYA" Bonyeza wanachukua taarifa zako

HATUA:

"PIN na OTP yako ni kama funguo za nyumba yako. USIMPE mtu yeyote kamwe, kwa sababu yoyote ile."

TAMBUA ISHARA ZA HATARI

Haraka-haraka, usiri, "ada" ya mapema, au faida zilizo nzuri sana kuliko uhalisia. Zote ni ishara za kuchukua tahadhari.

LINDA TAARIFA ZAKO

PIN na OTP ni siri. Usibonyeze linki za ajabu ,thibitisha kwenye namba rasmi pekee.

TOA TAARIFA

Waambie benki au wakala wako, wafungie namba hiyo na uwatahadharishe rafiki na familia yako dhidi ya utapeli na uhalifu huo.

MATOKEO

"Niliigundua, nikaifungia na nikautahadharisha mtaa mzima!.
"IMEFUNGIWA TULIA, KISHA THIBITISHA"

Ujumbe wowote unaokushinikiza? Tulia kwanza, Vuta pumzi, Thibitisha na kuhusu kampuni husika kwenye namba yao rasmi kabla hujachukua hatua."

USILIPE KAMWE ILI KUPOKEA ZAWADI

Kazi na mikopo ya kweli haviombi utume pesa kwanza. Kanuni hiyo pekee inazuia utapeli mwingi. "Si kila king'aacho ni dhahabu!"
"UMESHINDA" au **"FAIDA YA HARAKA"**? Tulia. Thibitisha. Usilipie kupokea pesa.

SIKU ZIJAZO (Baadaye haifiki kamwe)

HALI HALISI

"Siku zijazo? Ha! Nitawaza kuhusu hilo... siku hiyo itapofika!"

CHANGAMOTO

"Lakini uzee unamjia kila mtu... na vivyo hivyo ada za shule na siku ngumu. Uzee bila akiba ! Wakati sahihi zaidi wa kupanda mti ulikuwa miaka ishirini iliyopita. Wakati mwingine ni leo. Nivivyo hivyo kwa siku zako zijazo."

SIKU ZIJAZO

HATUA

"Panga vitu vikuu vitatu kwa ajili ya siku zijazo, mwanangu: navyo ni uzee, watoto wako na familia unayoiacha nyuma."

PANGA KWA AJILI YA SIKU ZIJAZO TATU

1. UZEE
2. WATOTO
3. FAMILIA

KUSTAAFU

Jiunge na mfuko wa pensheni (NSSF / PSSSF) au weka akiba yako mwenyewe. Anza kwa kuweka kigodogo, muda utafanya mengineyo.

ELIMU

Fungua akiba ya elimu mapema. Kiasi kidogo cha kila mwezi kinashinda taharuki kubwa yabaadaye.

FAMILIA YAKO

Andika wosia rahisi. Taja mrithi/mwasiliani wako wa karibu. Waambie familia mahali nyaraka zilipowekwa.

"TUKO TAYARI"

MATOKEO

Kila jirani alitaja lengo MOJA la siku zijazo, pensheni, mfuko wa elimu au wosia na akaanza mwezi huu.
Hatua ndogo, amani kubwa.

MUDA Ni RAFiKi YAKO
Jinsi unavyoanza mapema, ndivyo riba ya mseto inavyokufanyia kazi zaidi. Kidogo, kinachowekwa kando kwa miaka mingi, kinakuwa kingi kimyakimya.

LENGO MOJA, LEO
Usisubiri hadi uweze kupanga kila kitu. Chagua lengo moja la siku zijazo na uchukue hatua yakwanza kabisa ndogo sasa hivi.
"Mwenye kupanga, hupata."

TAJA LENGO MOJA la siku zijazo leo uzee, shule ya mtoto,au familia yako kisha anza.
Siku Zijazo

MSiMU MMOJA BAADAYE (Mtaa wa Faraja)

HONGERA!
Harakati ni zile zile. Mitazamo ni mpya. Tazama kilichobadilika.
•**TUMA**: Anagawanya mapato 50/30/20. Ana vibubu viwili vya pesa. Anaona faida halisi na anaiwekeza tena.
•**SKUDU**: Anaweka akiba kila wiki. Alinunua bodaboda MPYA ya 2 kwa mkopo, na kuepuka matapeli wa mikopo ya kausha damu.
•**ASHA**: Ana akaunti ya benki. Elimu ya fedha na Akiba kwa ajili ya watoto wake inakuwa.
•**DiTO**: Anauwezo wa kugundua na kuepuka utapeli. Anawekeza kiasi kidogo kila mwezi kwa ajili ya maisha ya baadaye.

"Mwenda pupa, hula embe bichi."

KANUNI 10 ZA PESA

Kata ukurasa huu. Ubandike mahali utakapouona kila siku.

1. Ipe kila shilingi kazi: Tenga bajeti kwa mfumo wa 50/30/20.
2. Jilipe wewe kwanza: Weka akiba kabla hujatumia.
3. Akiba haiozi: Hifadhi mfuko wa akiba ya dharura.
4. Weka pesa yako benki: Ni salama na inakuwa.
5. Linda PIN na OTP yako: Usimwambie mtu yeyote kamwe.
6. Kopa tu ili kujenga: Pata faida kubwa kuliko gharama ya mkopo.
7. Jikinge dhidi ya siku mbaya kwa bima: Afya kwanza.
8. Wekeza kidogo, dumu kwa muda mrefu: Uvumilivu unashinda mihemko/kelele.
9. Tenga pesa ya biashara na ya matumizi nyumbani: Andika kila kitu chini.
10. Panga kwa ajili ya siku zako zijazo leo: Uzee, watoto na familia

PESA NI AKILI

RAMANI YA PESA (Safari yako ya kifedha)

Kila safari ya kifedha inafuata barabara ile ile. Itembee kwa mpangilio hatua kwa hatua.

1. INGIZA: Mapato yanaingia
2. BAJETI: 50 / 30 / 20
3. WEKA AKIBA: Mfuko wa dharura kwanza
4. LINDA: Ngao ya bima
5. WEKEZA: Kuweka akiba kwa miaka mingi
6. PANGA: Jenga siku zako zijazo

Mahali popote ulipo kwenye barabara ya safari hii chukua tu hatua inayofuata. Hiyo ndivyo inavyotakiwa.

ZANA ZA USALAMA (Iweke hii karibu)

FUNGUA AKAUNTI

- Leta NIDA yako au Kitambulisho halali.
- Leta namba yako ya simu.
- Ulizia akaunti ya gharama nafuu.
- Weka PIN ya siri (sio mwaka wako wa kuzaliwa).
- Chukua kadi yako ya ATM na uitunze salama.
- Washa huduma ya ujumbe wa SMS (alerts).
- Hifadhi namba ya USSD ya benki.

USALAMA WA PESA ZA KWENYE SIMU

- Thibitisha JINA kabla hujatuma.
- Zihesabu sifuri kwenye kiasi unachotuma.
- Weka PIN na OTP yako siri.
- Hakuna wakala wa kweli anayeomba PIN yako.
- Jua ada na viwango vya mwisho vya kila siku.
- Hifadhi kila SMS kama risiti.
- Funga laini yako ya SIM kwa PIN.

ISHARA ZA HATARI ZA UTAPELI

- "Umeshinda!" lipa ada kwanza.
- Kukuharakisha au kukutisha.
- Mipango ya "Ongeza pesa yako maradufu".
- Kuomba PIN, OTP au namba ya siri.
- Linki za ajabu za kubonyeza.
- Faida zinazozidi kiasi kuwa za kweli.
- Unapokuwa na shaka tulia na uthibitishe.

MPANGO WAKO WA PESA (Jaza hapa!)
Mpango uliopo kichwani mwako ni wazo tu. Mpango uliopo kwenye karatasi ni ahadi. Chukua kalamu ukurasa huu ni wako.

PESA YANGU YA MWEZI (50 / 30 / 20)
Mapato yangu mwezi huu: TSh ____________
MAHITAJI YA LAZIMA (50%): TSh ____________
MAHITAJI YASIO LAZIMA (30%): TSh ____________
AKIBA (20%): TSh ____________

HATUA ZANGU 3 ZA KWANZA (Wiki hii)
1 ____
2 ____
3 ____

AHADI YANGU
Nitatawala na kusimamia pesa zangu, hatua moja ndogo kwa wakati mmoja. Pesa ni akili.
Sahihi: _______________________ Tarehe: ____________

UNAWEZA KUFANYA HILI.
Huhitaji kuwa tajiri ili uanze. Unahitaji tu kuanza hapo hapo ulipo. ANZA LEO

MAARIFA PESA

Kwa hisani ya TBA (Tanzania Bankers Association)

NIKOFIT NA MAARIFA PESA

Kila shilingi ina stori yake. Fanya yako iwe ya hekima.
Kutana na wakazi wa Mtaa wa Faraja ambao huwezi kuwasahau kirahisi; Tuma muuza chakula, Skudu dereva wa bodaboda, Asha fundi cherehani, Dito mjasiriamali mdogo, Bi Kijumbe bingwa wa kuweka akiba na mzee mwenye busara Papa Mfumo. Kwa pamoja wanakabiliana na changamoto zilezile za fedha zinazowakuta mamilioni ya Watanzania kila siku:

TBA
TANZANIA BANKERS ASSOCIATION

Physical Address:
Block 41, Kinondoni, Faykat Tower,
Alhassan Road, Dar es salaam, Tanzania.

Postal Address:
P.O.Box 70925, Dar es salaam, Tanzania.

Tel: 255-22-2127764 | Fax: 255-22-2124492
Email: info@tanzaniabankers.org
Web: www.tanzaniabankers.org